

TAARIFA YA UTEKELEZAJI UJENZI WA BARABARA YA KILONGAWIMA – KUNDUCHI.

Barabara ya Kilongawima – Kunduchi ina urefu wa **km 2** na ni miongoni mwa barabara zilizo katika Fungu la pili zenye jumla ya urefu wa **km 11** ikiwa na gharama ya **Shilingi 28,978,993,880.51**. Mkandarsi mjenzi wa Mradi huu ni “**China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC)**”. Ujenzi wa Mradi huu ulianza rasmi tarehe **28 Oktoba 2017** na unatarajiwa kukamilika tarehe **28 Agosti 2019**. Kwa ujumla kazi zinazoendelea kufanyika katika barabara hii ni ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami urefu wa **km 2**, ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua wenye upana wa **mita 1.1**, ujenzi wa makalavati **sita (6)** yenye ukubwa wa **mita 0.9** na urefu **mita 10** (pipe culverts) kila moja, Ujenzi wa kalvati (Box culvert) lenye upana wa **mita 2** na kina mita **1.2**, Ujenzi wa kalvati (Box culvert) lenye matundu mawili (double cell) yenye upana wa **mita 4** na kina **mita 1.2** kila moja, uwekaji wa taa zinazotumia nguvu ya jua (Solar Street Lights) na ujenzi wa njia za watembea kwa miguu zenye upana wa **mita 1.5**.

Mradi huu unajengwa kwa gharama ya Shilingi **Bilioni mbili, milioni mia tisa thelathini na tisa, laki sita sabini na tano, mia tano ishirini na saba (Shilingi 2, 939, 675,527.00)** ambapo malipo yaliyofanyika mpaka sasa ni Shilingi **Bilioni moja, milioni mia nane kumi na nane, laki sita tisini na mbili, mia tano thelathini na senti sita (Shilingi 1, 818, 692,530.06)** Fedha hizo Mkopo kutoka Benki ya Dunia kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Manufaa ya Mradi huu wa Barabara ya Kilongawima – Kunduchi ni pamoja na;

- Kusaidia kupunguza msongamano wa magari kwenye barabara mpya ya Bagamoyo (New Bagamoyo Road)
- Kusaidia kupunguza mafuriko kutokana na ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua na makalvati.
- Kuongeza Usalama zaidi kwa wanaanchi na mali zao hasa wakati wa usiku kwa sababu barabara hii itawekwa taa za barabarani zinazotumia Nishati ya jua (**Solar Street Lights**).
- Kusaidia kupunguza ajali kwa kiasi kikubwa kwa kuwa zitajengwa sehemu za watembea kwa miguu zilizotenganishwa na sehemu vinapopita vyombo vya Usafiri.

PICHA ZA MRADI WA BARABARA YA KILONGAWIMA-KUNDUCHI

